

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na:MTC/I.20/2/153

17/05/2021.

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

NAFASI YA AJIRA YA KADA YA MTENDAJI WA KIJIKI

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Makambako, anapenda kuwatangazia wataanzania wote wenye sifa, kuomba nafasi wazi ya Ajira ya Mtendaji wa Kijiki nafasi tano (5) katika masharti ya kudumu.

AFISA MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III: NAFASI 5 (VILLAGE EXECUTIVE OFFICER III)

SIFA ZA MWOMBAJI:

1. Awe na elimu ya kidato cha nne au sita.
2. Awe amehitimu mafunzo ya Astashahada/cheti (NTA level 5) katika moja ya fani zifuatazo:-
Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au Chuo chochote kinachotambulika na Serikali.
3. Awe na umri usiozidi miaka 45.

KAZI NA MAJUKUMU:

- (i) Afisa Masuuli na Mtendaji wa Serikali ya Kijiki.
- (ii) Kusimamia Ulinzi na Usalama wa raia na mali zao kuwa mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala bora katika Kijiki.
- (iii) Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiki.
- (iv) Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiki.
- (v) Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu.
- (vi) Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na

- kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati kama vile kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali.
- (vii) Kiongozi wa Wakuu wa vitengo vya kitaalam katika kijiji.
 - (viii) Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Kijiji.
 - (ix) Mwenyekiti wa kikao cha wataalam waliopo katika kijiji.
 - (x) Kusimamia utungaji wa sheria ndogo za kijiji.
 - (xi) Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wannchi.
 - (xii) Atawajibika kwa Afisa Mtendaji wa Kata.

NGAZI YA MSHAHARA:

TGS B1, Tshs.390, 000/= kwa mwezi.

**MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI WOTE AMBAYO NI YA
LAZIMA KUZINGATIWA:**

- 1.Mwombaji ni lazima awe ni raia wa Tanzania.
- 2.Awe hajawahi kufungwa kwa makosa ya jinai.
- 3.Awe hajawahi kupunguzwa/kufukuzwa kazi Serikalini.
- 4.Maombi ni lazima yaambatanishwe na vivuli vya vyeti vya kuzaliwa, kuhitimu Elimu ya Sekondari na vyo vya mafunzo/taaluma.
- 5.Awe na Umri usiozidi miaka 45.
- 6.Maombi lazima yaambatanishwe na picha 2 za Passport size za hivi karibuni(zilandikwe majina kwa nyuma).
- 8.Maombi lazima yaambatanishwe na Wasifu binafsi (CV) zenye wadhamini wawili na mawasiliano ya uhakika, Anuani, barua pepe na namba za simu.
- 9.Awe hajaajiriwa wala hajawahi kuajiriwa Serikalini.
- 10.Awe na umri wa zaidi ya miaka 18.
11. Hati za matokeo za kidato cha nne, kidato cha sita na za vyeti vya Taaluma hazitapokelewa
12. Watumishi wa Umma walioajiriwa wahakikishe wanapitisha maombi yao kwa Waajiri wao
13. Watakaoitwa kwenye usaili watajigharamia wenyewe
14. Maombi yanaweza kuandikwa kwa kutumia lugha ya Kiswahili au Kiingereza
14. Awe tayari kufanya kazi eneo lolote atakalopangiwa ndani ya Halmashauri ya Mji Makambako.

MAOMBI YOTE YATUMWE KWENYE ANUANI IFUATAYO:-

MKURUGENZI,
HALMASHAURI YA MJI,
S.L.P 405,
MAKAMBAKO.

MWISHO WA KUTUMA MAOMBI NI TAREHE 30/05/2021

TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA:



Paulo S. Malala
MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA MJI
MAKAMBAKO.

MKURUGENZI
HALMASHAURI YA MJI
MAKAMBAKO

Halmashauri ya Mji Makambako, Mtaa wa Sigrid, Barabara kuu ya Njombe, S.L.P 405 Makambako, Njombe, Nukushi Na:
026-2968891, Simu Na: 026-2968892,
Barua Pepe: td@makambakotc.go.tz, Tovuti: www.makambakotc.go.tz